

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA WAZIRI MKUU  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



UTAYARISHAJI WA MRADI,  
UKADIRIAJI WA UWEKEZAJI,  
TATHMINI YA ATHARI YA MAZINGIRA NA  
SERA YA HIFADHI

HAIUZWI

MWONGOZO KWA WASHIRIKI WA SERIKALI ZA MITAA

NGAZI YA CHINI

Katibu Mkuu,  
Ofisi ya Waziri Mkuu,  
Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI),  
S.L.P 1923,  
DODOMA.

Tarehe: Aprili 2006

## **DIBAJI**

Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ina wajibu wa kutambua kuendelea kuwepo kwa mapungufu katika uwezo wa nguvukazi (rasilimali watu), hususan katika eneo la utayarishaji miradi, tathmini ya uwekezaji, na ukadiriaji wa hifadhi ya mazingira, kupitia serikali ya mitaa ya Tanzania. Kwa hali hiyo Wizara ya Tawala za Mikao na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kupitia mradi wa maboresho ya Serikali za Mitaa (LGSP), hufanyakazi ya ushauri kwa wadau (wabia) wa maendeleo, mwongozo huu umetayarishwa ili utumike katika mafunzo ya wafanyakazi mameneja na watawala wa ngazi za chini wa Tawala za Serikali za mitaa katika Wilaya zote za Tanzania.

Madhumuni ya mafunzo haya ni kuwapa fursa maofisa wa serikali za mitaa kupata maarifa sahihi na kujiamini katika njia za utayarishaji wa miradi na tathmini ya uwekezaji. Seti hii ya maarifa tofauti, kwa kiwango kikubwa itaboresha ufanisi wa ubainishaji wa rasilimali za Wilaya na kuongeza matarajio ya matokeo ya uwekezaji wa umma. Matarajio yaliyolengwa yatajumuishwa kupunguza athari za umasikini kwa kujenga miundombinu kama vile barabara ili kurahisisha mawasiliano na kuyafikia masoko, kuongeza/kuboresha upatikanaji na kunufaika na maji safi na salama na utoaji wa elimu ya msingi na huduma za afya kwa wote.

Mbinu za utayarishaji wa mrasdi na tathmini ya uwekezaji na maelezo mazuri ya utekelezaji katika mwongozo huu wa mafunzo, zinatarajiwa kuboresha uwezo wa kubainisha rasilimali muhimu katika harakati za kuleta maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi katika asasi mbalimbali na watumishi wa serikali za mitaa, kuboresha ubora wa maisha kwa Tanzania nzima.

**YALIYOMO:**

<b>DIBAJI .....</b>	<b>i</b>
<b>YALIYOMO .....</b>	<b>ii</b>
<b>VIFUPISHO .....</b>	<b>iv</b>
<b>1.0 UTANGULIZI NA USULI WA MAFUNZO... ..</b>	<b>1</b>
1.1 MUHTASARI WA MTAALA WA MAFUNZO .....	2
<b>2.0 MODULA 1. UTAYARISHAJI WA MRADI .....</b>	<b>4</b>
2.1 KIKAO 1: UTANGULIZI .....	4
2.1.1 MADHUMUNI YA JUMLA .....	4
2.1.2 MADHUMUNI MAHSUSI .....	4
2.1.3 MADHUMUNI YA MAFUNZO.....	
2.1.3 KUTAFSIRI UTAYARISHAJI WA MRADI NA TATHMINI YA UWEKEZAJI.....	5
2.1 KIKAO 2: SERA KATIKA MAHALI, MUUNDO WA TAASISI NA MFUMO WA KISHERIA. ....	6
2.2.1 SERA YA MAHALI .....	6
2.2.2 MUUNDO WA TAASISI .....	7
2.2.3 MFUMO WA KISHERIA .....	8
2.3 KIKAO 3: UZOEFU WA WASHIRIKI, MAJADILIANO, MAFUNZO YALIYOPATIKANA .....	8
<b>3.0 MODULA 2: MCHAKATO WA TATHMINI YA MRADI .....</b>	<b>9</b>
3.1.1 MADHUMUNI YA JUMLA YA KIPIMO HIKI .....	9
3.1.2 MADHUMUNI YA MAFUNZO.....	
3.2. KIKAO 1: UTAMBUZI WA MRADI NA UCHUNGUZI YAKINIFU .....	9
3.2.1 ASILI NA UTAMBUZI WA MRADI .....	9
3.2.2 USHIRIKISHAJI ASILIA WA UTAYARISHAJI MRADI .....	10
3.2.3 MFUMO WA KIMANTIKI KAMA ZANA YA KUBAINISHA MAENEO MUHIMU YA MRADI .....	11
3.2.4 UCHUNGUZI YAKINIFU .....	13

3.3 KIKAO 2: MZUNGUKO WA MRADI KATIKA MUUNDO WA SERIKALI ZA MITAA .....	14
3.3.1 MAKUBALIANO JUU YA MWONEKANO WA MZUNGUKO WA MRADI.....	14
3.3.2 HATUA ZA MZUNGUKO WA MRADI.....	15
3.4 KIKAO 3: MCHANGANUO WA MRADI KIUFUNDI, KIUCHUMI, KIFEDHA, KIJAMII NA KIMAZINGIRA.....	16
3.4.1 UKADIRIAJI WA UKUBWA WA MRADI .....	16
3.5 KIKAO 4: VIPENGELE VYA UTEKELEZAJI MRADI, USIMAMIZI NA TATHMINI.....	21
3.5.1 UTEKELEZAJI WA MRADI .....	21
3.5.2 USIMAMIAJI NA TATHMINI YA MRADI.....	22
<b>4.0 KIPIMO 3: UKADIRIAJI WA ATHARI MAZINGIRA NA SERA ZA HIFADHI .....</b>	<b>23</b>
4.1.1 MALENGO YA JUMLA YA KIPIMO HIKI.....	23
4.1.2 MALENGO YA MAFUNZO.....	
4.2 KIKAO 1: MTAZAMO JUU YA MAZINGIRA NA TATHMINI YA ATHARI ZA MAZINGIRA NA SERA YA HIFADHI (EIA) .....	23
4.2.1 UTAMBULISHO KUHUSU ATHARI ZA MAZINGIRA NA MAHITAJI YAKE.....	24
4.2.2 SHERIA NA MFUMO WA KISERA KUHUSU USIMAMIZI MAZINGIRA.....	25
4.2.3 UKUBWA WA MAZINGIRA.....	26
4.2.4 UTAMBULISHO NA TATHMINI YA ATHARI ZA KIMAZINGIRA NA UMUHIMU WAKE.....	27
4.2.6 HATUA ZA KUPUNGUZA MAKALI.....	
4.2.5 UKADIRIAJI WA ATHARI – CHIMBUKO NA UMUHIMU.....	
4.2.7 WAJIBU WA WASHIKA DAU KATIKA USIMAMIAJI WA MAZINGIRA NA MAPITIO YA EIA.....	
<b>5.0 KIPIMO 4: UCHUNGUZI KIFANI JUU YA UTATHMINI WA MRADI NA TATHMINI YA MAFUNZO.....</b>	<b>28</b>
5.1.1 MALENGO YA JUMLA YA KIPIMO HIKI.....	28
5.2 KIKAO 1: UCHANGANUZI WA MRADI.....	28
5.3 KIKAO 2: MAPITIO YA MAFUNZO YA SIKU YA 1, 2, 3 NA 4.....	28
5.4 KIKAO 3: TATHMINI YA MAFUNZO.....	28
<b>6.0 KIAMBATISHO: FAHARASA .....</b>	<b>29</b>

## VIFUPISHO

ABPs	Area Based Programs (Mipango Kutegemeana na Eneo)
ARCBP	Annual Report and Capacity Building Plan (Ripoti ya Mwaka na Mpango wa Kujenga Uwezo)
ARSIP	Annual Report and Service Improvement Plan (Ripoti ya Mwaka na Mpangowa wa Kuboresha Huduma)
CBG	Capacity Building Grant (Msaada wa Kujengea Uwezo)
CDG	Capital Development Grant (Mtaji wa Kujengea Uwezo)
CMT	Council Management Team (Timu ya Halmashauri ya Menejimenti/Utawala)
DADs	District Agriculture Development (Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya)
DANIDA	Danish International Development Agency (Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa ya Denmark)
DAS	District Administrative Secretary (Katibu Tawala wa Wilaya)
DC	District Commissioner (Mkuu wa Wilaya)
DED	District Executive Director (Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya)
DF	District Facilitators (Wawezeshaji wa Wilaya)
DFID	Department for International Development (Idara ya Maendeleo ya Kimataifa)
DMT	District Management Team (Timu ya Management/Utawala wa Wilaya)
DPLO	District Planning Officer (Ofisa Mipango wa Wilaya)
DSAs	Daily Substance Allowance (Posho ya Kila Siku ya Kujikimu)
FINNIDA	Finnish Development Agency (Wakala wa Maendeleo wa Ufini)
GOT	Government of Tanzania (Serikali ya Tanzania)
BLG	Higher Local Government (Serikali Kuu ya Mtaa)
HoD	Heads of Department (Mkuu wa Idara)
IPF	Indicative Planning Figure (Michoro ya Viashiria vya Mpango)
LGA	Local Government Authority (Mamlaka ya Serikali za Mtaa)
LGCDG	Local Government Support Programme Grant (Msaada a Mtaji wa Maendeleo ya Serikali ya Mtaa)
LGRP	Local Government Reform Programme (Mpango wa Maboresho wa Serikali za Mtaa)
LGSP	Local Government Support Programme (Mpango wa Kusaidia Serikali za Mtaa)
LLG	Lower Level Government (Ngazi ya Chini ya Serikali)
MEO	Mtaa Executive Officer (Ofisa Mtendaji wa Mtaa)
MOF	Ministry of Finance (Wizara ya Fedha)
MTEF	Medium Term Expenditure Framework (Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati)
MTPB	Medium Terms Plan and Budget (Mpango wa Bajeti wa Muda wa Kati)
NF	National Facilitators (Wawezeshaji wa Kitaifa)
NGO	Non Governmental Organisation (Jumuia Isiyo ya Kiserikali)
O&OD	Opportunities and Obstacles to Development (Fursa na Vikwazo vya Maendeleo)
PMG	Performance Budgeting (Bujeti ya Utendaji/Uendeshaji)
POPP	President's Office Planning and Privatisation (Ofisi ya Rais, Mipango ya Ubinafsishaji)

PORALG	President's Office Regional Administration and Local Government (Ofisi ya Raisi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mtaa)
RAS	Regional Administrative Secretary (Kamati ya Ushauri ya Mkoa)
RC	Regional Commissioner (Mkuu wa Mkoa)
RCC	Regional Consultative Committee (Kamati ya Ushauri ya Mkoa)
RNE	Royal Netherlands Embassy (Ubalozi wa Kifalme wa Uholanzi)
RRWSS	Rural Water Supply & Sanitation (Usambazji Maji Safi na Taka Vijijini)
SIDA	Swedish International Development Agency (Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa wa Uswidi)
SNV	Dutch Development NGO (Maendeleo ya Jumuiia Isiyo ya Kiserikali ya Ujerumani)
TASAF	Tanzania Social Action Fund (Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania)
UAPP	Urban Authority Partnership Project (Mradi wa Umoja wa Mamlaka ya Mji)
UNCDF	United Nations Capital Development Fund (Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo ya Mitaji)
UNICEF	United Nation Children and Education Fund (Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto na Elimu)
VA	Village Assembly (Mkutano wa Kijiji)
VC	Village Council (Halmashauri ya Kijiji)
VEO	Village Executive Officer (Ofisa Mtendaji wa Kata)
WDC	Ward Development Committee (Kamati ya Maendeleo ya Kata)
WF	Ward Facilitators (Wawezeshaji wa Kata)

## **1.0 UTANGULIZI**

Mafunzo haya yanaangalia juu ya misingi ya utayarishaji wa mradi, stadi na mbinu muhimu za ukadiriaji wa uwekezaji katika mzunguko wa mradi. Vifaa vya mafunzo vilivyowasilishwa katika mwongozo huu vinalenga wafanyakazi wa managementi na utawala katika ngazi za Serikali za Mitaa. Sehemu hii imeandaliwa ili kutosheleza kazi na huduma za Serikali za Mitaa kwa ngazi ya Wilaya, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 145 na 146 na Sheria ya Serikali ya Mitaa Na. 7,8,9 za mwaka 1982 na sheria anuwai ya 2000.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali za Mitaa Kifungu cha Sheria na. 7-9 ya mwaka 1982 kinaruhusu na kusaidia utekelezaji wa kanuni za Serikali za kupeleka Madaraka Mikoani. Kipindi cha 1992 – 2002 kilikuwa ni cha maboresho katika sekta ya jamii. Maboresho hayo yalilenga kuongeza ufanisi na kupata huduma yenye tija kwa jamii ya Watanzania. Maboresho haya yalikuwa na madhumuni ya kubadili majukumu ya Serikali Kuu kutoka katika kujishughulisha moja kwa moja katika uzalishaji na upokeaji huduma, hadi katika muundo wa sera, ushirikishaji, ushauri, uimarishaji uwezo wa mamlaka za Serikali za Mitaa (LGA), kuhakikisha amani na ulinzi kwa kutengeneza mazingira ya uwezeshaji wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuweza kufanya vizuri.

Hatimaye, mchakato wa kupeleka Madaraka Mikoani kwa kweli umepanua na kuhamishia mamlaka, kazi na wajibu wa Serikali Kuu katika wilaya na ngazi za chini. Serikali za Mitaa sasa hivi zina nguvu na zimeanza kutekeleza mipango ya maendeleo ambayo inatokana na vipaumbele vya maeneo husika. Vipaumbele hivyo hujumuisha mambo yafuatavyo:

Kundi 1	Ukuaji na Upunguzaji wa Umaskini wa kipato
Lengo la 1	Kuhakikisha usimamizi mzuri wa uchumi
Lengo la 2	Kuchochea ukuaji mpana na endelevu
Lengo la 3	Kustawisha na kuendeleza upatikanaji wa chakula ngazi ya familia kwa maeneo ya mijini na vijijini.

Lengo la 4	Kupunguza umaskini wa kipato kwa wanaume na wanawake maeneo ya vijijini
Lengo la 5	Kupunguza umaskini wa kipato kwa wanawake na wanaume maeneo ya mijini

Kundi 2	Uboreshaji wa maisha ya Jamii
Lengo la 1	Kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora ya msingi na Sekondari kwa wavulana na wasichana, elimu ya watu wazima kwa wanawake na wanaume, na kupanua elimu ya juu pamoja na mafunzo ya ufundi
Lengo la 2	Kuoboresha uhai,afya, na maisha kwa wanawake na watoto wote hasa wale waishio katika mazingira magumu
Lengo la 3	Upatikanaji wa maji safi na salama, mfumo wa maji taka, makazi bora na mazingira endelevu na salama na hivyo kupunguza madhara yatokanayo na athari za mazingira.
Lengo la 4	Kutoa ulinzi wa kutosha na haki za kijamii kwa walio katika mazingira hatari, na makundi ya wahitaji kwa kuwapa mahitaji na huduma muhimu.
Lengo la 5	Kuhakikisha utaratibu unaofaa kwa kutoa hudumu bora za kijamii ambazo wanazimudu na zinapatikana.

Madhumuni ya mchakato wa Madaraka Mikoani ni kuanzisha mfumo wa utawala ambao utaunda Mamlaka ya Serikali kuu na Serikali za Mitaa, na Serikali ambazo zina ufanisi, tija, uwezeshaji na utoaji wa huduma bora kwa Watanzania wote. Madhumuni Makuu ya mchakato wa Madaraka Mikoani ni kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuainisha miundo mbinu muhimu na kutoa huduma za ustawi wa jamii kwa watu, kwa kupitia mbinu shirikishi iliyojikita katika misingi ya uwazi na uwajibikaji.

Muongozo huu unatoa misingi ya upatikanaji wa stadi za kitaalamu ambazo ni muhimu mno katika kumudu mzunguko wa mradi, ikiwemo kuutambua mradi, upembuzi yakinifu, maandalizi, hatua za tathmini na baadhi ya misingi ya utekelezaji wa mradi,



usimamizi na tathmini. Shughuli hizi za mradi – mchakato unafikiria mbinu shirikishi ambazo hujikita katika kupata maoni ya kuwanufaisha walengwa katika mchakato mzima wa mradi. Mbinu hizi zimelenga kuzidisha dhana ya umiliki na kuhakikisha uendelezaji wa mipango ya muda mrefu ya miradi inayofadhiliwa kwa rasilimali chache za jamii. Serikali ya Tanzania imeonyesha

kuwajibika kwake katika kuendeleza ushiriki wa wadau wote katika mipango ya maendeleo kwa kupitia sera mbalimbali na uanzishaji, ambao unasisitiza hoja na umuhimu wa mpango shirikishi.

### 1.1 MUHTASARI WA MTAALA WA MAFUNZO

Mafunzo kuhusu uandaaji wa mradi, tathmini ya uwekezaji na ukadiriaji kuhusu athari za mazingira ndani ya Serikali za mitaa, yatapaswa kufuata mtaala wa mafunzo na utaratibu kama inavyoonyeshwa hapa chini:

MODULA I	Uandaaji wa mradi	Mada
Kikao cha I	Utangulizi na Usuli wa mafunzo	
Sehemu I	Utangulizi	Dakika 60
Sehemu 2	Madhumuni ya Modula	Dakika 60
Sehemu 3	Tafsiri ya Istilahi	Dakika 60
Jumla ya muda wa kikao		Saa 3
Kikao cha 2	Sera, Muundo wa Taasisi na mfumo wa kisheria	
Sehemu ya I	Mapitio ya Sera zilizopo na mambo mengine yanayoweza kufikiwa	Dakika 60
Sehemu ya 2	Muundo wa Taasisi na mfumo wa kisheria	Dakika 60
Jumla ya muda wa kikao		Saa 2
Kikao cha 3	Uzoefu wa Washiriki Majadiliano kuhusu masomo waliyojifunza	Dakika 60
Muda wa kikao		Dakika 60

<b>Modula 2</b>	<b>Mchakato wa mchanganuo wa mradi</b>	<b>muda</b>
Kikao 1	Utambuzi wa mradi na uchunguzi yakinifu	
Sehemu 1	Hali ya mradi na utambuzi wake	Dakika 30
Sehemu 2	Hali ya ushirikishwaji katika utambuzi wa mradi	Dakika 30
Sehemu 3	Uchambuzi wa kimantiki kama nyenzo katika uandaaji wa mradi	Dakika 60
Jumla ya muda wa kikao		Saa 2
Kikao 2	Mzunguko wa mradi ndani ya muundo wa serikali za mitaa	
Sehemu 1	Muonekano wa hatua za mzunguko wa mradi ndani ya mzunguko wa mradi	Dakika 30
Sehemu 2	Hatua ndani ya mzunguko wa mradi	Dakika 30
Jumla ya muda wa kikao		Saa 1
Kikao 3	Vipengele vya Uchambuzi wa mradi	
Sehemu 1	Ukubwa wa uchambuzi wa mradi	Dakika 20
Sehemu 2	Uchambuzi wa ki-ufundi	Dakika 20
Sehemu 3	Uchambuzi wa kiuchumi na kifedha	Dakika 30
Sehemu 4	Uchambuzi wa kimazingira na kijamii	Dakika 20
Sehemu 5	Mambo ya hatari katika uchambuzi wa mradi	Dakika 30
Jumla ya muda wa kikao		Saa 2

<b>MODULA 3</b>	Ukadiriaji wa Athari za kimazingira na Sera ya Hifadhi	Muda
Kikao 1	Maelezo kuhusu mazingira na EIA	
Sehemu 1	Utangulizi kuhusu EIA na umuhimu wake	Dakika 60
Sehemu 2	Ukadiriaji athari: Chimbuko na umuhimu wake	Dakika 60
Sehemu 3	Hatua za kupunguza makali katika EIA	Dakika 30
Sehemu 4	Wajibu wa washikadau katika usimamizi wa mazingira na mapitio ya EIA	Dakika 30
Jumla ya muda wa kikao		Saa 3

<b>MODULA 4</b>	Uchunguzi kifani wa uchanganuzi wa mradi	Muda
Kikao 1	Kuhusu uchanganuzi wa mradi	Saa 2
Jumla ya muda wa kikao		Saa 2

## **2.0 MODULA 1: MAANDALIZI YA MRADI**

### **2.1 KIKAO 1: UTANGULIZI NA USULI WA MAFUNZO**

#### **2.1.1 Madhumuni ya Jumla**

Madhumuni ya jumla ya mwongozo huu ni:-

1. Kuendeleza na kuboresha mbinu za ukadiriaji wa mradi zitakazotumika katika ngazi za chini za Serikali za Mitaa.
2. Kuwasaidia maofisa katika kufikia ubainishaji yakinifu wa rasilimali;
3. Kukomesha upotevu wa rasilimali adimu

#### **2.1.2 Madhumuni Mahsus**

Katika mchakato wa kupanga, kuunda na kukadiria miradi ya maendeleo ya Wilaya, madhumuni yafuatayo yanatoa miongozo muhimu.

- i. Kutambua na kutumia vigezo muhimu katika ukadiriaji mradi ukijumuisha kuzingatia ufundi, uchumi, jamii, mazingira na mahitaji ya kifedha, sambamba na mchanganuo wa gharama na faida ili kubaini mapato sahihi katika uwekezaji husika;
- ii. Kufahamu umuhimu na ushirikishaji wa mazingira ambamo mradi unakadiriwa, ikijumuisha alengo ya Sera ya Taifa, mfumo wa kisheria, takwimu za msingi, mahitaji ya jamii, na malengo ya mpango wa Maendeleo ya Wilaya, katika mzunguko wa mradi;
- iii. Kutumia njia za ushirikishaji katika kukadiria mradi kwa kuzingatia vipaumbele na uteuzi wa mradi ukisaidiwa na wanufaika walengwa.
- iv. Kutayarisha, kuwasilisha na kulinda ripoti ya tathmini kwa kufanya maamuzi katika kamati husika na au halmashauri.

Kama ilivyobainishwa katika mtaala, mafunzo haya yanatakiwa kutolewa kwa muda wa siku nne. Siku tatu za mwanzo zitachukua saa sita na saa tatu tu katika siku ya mwisho. Mafunzo haya yanawalenga maofisa wa chini wa Serikali za Mitaa katika Wilaya, Halmashauri za Wilaya, na maofisa kutoka katika asasi nyingine ambazo zinahusiana nazo

### **2.1.3 Madhumuni ya Mafunzo**

Mwishoni mwa Modula hii washiriki watakuwa na uwezo wa:-

(i) Kuelewa muundo wa Taasisi na umuhimu wake, na kuunganisha nyaraka za Sera ya Taifa na

malengo pamoja na taratibu za kisheria katika maandalizi ya mradi.

(ii) Kuanzisha mpango wa jinsi gani watatumia stadi na maarifa waliyojifunza kwenye kazi

zao pamoja na kuwashirikisha wengine.

### **2.1.4 Kutafsiri Maandalizi ya Mradi na tathmini ya Uwekezaji**

Maandalizi ya mradi na tathmini ya uwekezaji, unatafsiriwa kwamba ni tathmini ya kina ya uhusiano, kutekelezeka, na kupatikana kwa matokeo tarajiwa katika wazo au pendekezo la mradi huo. Hujumuisha kupitia matokeo ya upembuzi yakinifu, kuthibitisha na kubainisha mchakato ambao utathibitisha na pale inapobidi, kurekebisha. Madhumuni ya mradi, ukubwa, mawanda, njia za utekelezaji na mifano, muda wa utekelezaji pamoja na kuzingatia mahitaji na mrekebisho ya kiufundi, kifedha, kiuchumi, kitaasisi, kimazingira, kijamii na kiusambazaji.

#### **Mchoro 1 – Hatua za maandalizi ya mradi**

Ndani ya Mpango wa Marekebisho ya Serikali za Mitaa (LGRP) Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unachukua hatua ya kupeleka utawala wa Madaraka Mikoani ambapo Serikali za Mitaa zinawajibika, katika maeneo yao ya utawala wa kisheria, kwa kufanya mambo yote ya mamlaka ya kisiasa, kiutawala na kifedha kama inavyoaminika kwamba inakidhi upatikanaji huduma bora kwa watu wote. Mamlaka haya hujumuisha kufanya maamuzi katika mambo ya mitaji na miundo mbinu ya uwekezaji.

Mamlaka ya mawakala ndani ya serikali (Kamati ya Bodi ya Tenda na Tathmini ya Kiufundi), pamoja na mambo mengine wana wajibu wa kufanyakazi ya uwakala wa kazi –mradi katika ngazi za Serikali za Mitaa.

Katika kufanya kazi hii kwa ufanisi mkubwa, wanakamati wa Mamlaka ya Mawakala wanatakiwa kupewa mafunzo kuhusu dhana ya miradi mizuri, ubunifu, kuunda na kukadiria njia, ambapo thamani kwa fedha itajulikana kwa kuzingatia kuingilia kati kwa uwekezaji katika ngazi ya Wilaya. Mafunzo katika ukadiriaji wa njia za mradi, na njia bora za utekelezaji, ambazo hujumuisha mambo yote ya msingi katika mradi mzima kuanzia mwanzo hadi katika tathmini ya matokeo. Uwekezaji wa kijamii katika elimu, afya, maji safi na salama pamoja na mwekezaji wa kiuchumi katika miundo mbinu ya usafirishaji hususan katika barabara za vijijini, madaraka na masoko ya vijijini ni muhimu mno katika mapambano dhidi ya umaskini. Mafunzo yanalenga kushirikisha michango na pia ushiriki katika ngazi ya Wilaya. Lengo mahsusi ni ubora wa misingi ya ukadiriaji wa mradi ambao utaboreshwa kwa maana ya kupata mahitaji ya tathmini, mawanda, njia sahihi na vipaumbele vizuri.

## **2.2 KIKAO 2: SERA YA MAHALI, MUUNDO WA ASASI NA MFUMO WA KISHERIA**

<b>Madhumuni ya Kikao</b>
<b>Kutathmini sera zilizopo, muundo wa asasi, na mfumo wa kisheria ulioshirikishwa na mbimu bora za ukadiriaji wa sera.</b>

### **2.2.1 Sera ya Mahali (Nafasi ya Sera)**

Katika kukadiria sera ya uwekezaji na jamii, kuna mfumo wa sera kisheria ambao unaongoza shughuli hizo; Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali za Mitaa sheria Na. 7,8 na 9 ya mwaka 1982, pamoja na sheria anuwai ya 2000, unatoa kumbukumbu za kisheria katika mchakato wa shughuli za uwekezaji na utayarishaji/ukadiriaji wa miradi. Mwongozo mwingine wa sera na chombo cha msingi katika kukadiria mradi na uwekezaji ni pamoja na:-

- i. Mkakati wa Taifa wa kukua na kupunguza umaskini (NSGRP) ni mfumo wa Kitaifa wa kupanga mwelekeo kuhusu upunguzaji umaskini na kuuweka katika agenda ya maendeleo ya nchi. NSGRP inatoa mwelekeo wa Taifa wa njozi za maendeleo (Vision 2025) kuhusu ukuaji wa ushirikiano, maisha bora, Umoja utulivu na amani, utawala bora, elimu bora na ushindani Kimataifa. Hii imo katika mipango ya milenia ya malengo ya maendeleo (MDG) kama ilivyokubaliwa Kimataifa kuhusu mikakati ya kupunguza umaskini, njaa, magonjwa, ujinga, uharibifu wa mazingira na udhalilishaji wanawake ifikapo 2015. Hii ni pamoja na kupanua wigo kwa nchi kumiliki na kushirikisha vyama vya kiraia (AZISE), maendeleo ya sekta binafsi, na ushirikiano wa ndani na nje ambao utazaa matunda kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. NSGRP inaeleza mikakati kuhusu upunguzaji umaskini (2000/01 – 02/03), marekebisho ya PRSP, mipango ya muda wa kati, ya ukuaji na upunguzaji umasikini na mpango wa Tanzania wa Mini –Tiger 2020 (TMTP -2020), ambao unatilia mkazo msukumo wa ukuaji ili kufikia lengo na mikakati ya njozi za 2025.

- ii. Mpango wa Maendeleo wa Tanzania 2025 ambao unatamka kwamba juhudi za Halmashauri lazima ziwawezeshe watu na kuchochea ushiriki wa umma na wa kidemokrasia. Mpango huo inabidi uwezeshe Serikali za Mitaa na jamii na kuendeleza misingi ya ushiriki  
  
katika kuhamasisha juhudi za kunufaika na rasilimali zilizopo, maarifa na uzoefu pamoja na kuchochea juhudi katika ngazi zote za jamii.
- iii. Rasimu ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini inayoelekeza jitihada za kupunguza umasikini nchini ili kupunguza umasikini uliokithiri kwa asilimi hamsini (50%) hadi ifikapo mwaka 2010 kwa kupitia njia za kukuza uchumi na kipato cha mtu, utoaji wa elimu, maji, huduma ya afya, nyumba bora, miundombinu na ajira. Vitu hivi vinahitaji uwekezaji mkubwa katika jamii;
- iv. Sheria ya Serikali za mitaa Na. 7-12 ya 1982 inafafanua kwa ufasaha nguvu na wajibu na kazi za ngazi mbalimbali katika Serikali za Mitaa katika utoaji wa huduma.
- v. Sera ya Taifa ya Mazingira 1997

**Marejeo mengine:**

- i. O & OD Community Participatory Planning – handbook, 2004 and Guidelines.
- ii. Guidelines for Preparation of Medium Term Plan and Budget Framework for 2004/05-  
2006/07 and MTEF
- iii. District Health Planning Guidelines 1998,
- iv. District Agriculture Development Planning Guidelines, 2002,
- v. National Framework Participatory Planning and Budgeting in LGAs, 2000 (Draft).
- vi. Planning Guidelines for villages and Mitaa, October 2004, and
- vii. Rural Development Policy 2003.



### **2.2.2 Muundo wa Taasisi**

Muundo wa Taasisi una uhusiano mkubwa na wajibu kwa wadau (kama vile Serikali za Mitaa, wafadhili, makandarasi, mabenki, wanufaika, mamlaka za sheria kama vile mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Baraza la Taifa la uhifadhi Mazingira, kwa mradi fulani ambao unatarajiwa kuwekezwa, ikiwemo kuorodhesha mikondo ya ushirikiano, ushirika na mifano mingine ya ushirikiano. Kwa mfano, mradi unaweza kubainishwa katika ngazi ya wilaya ndogo na kisha kuidhinishwa na Halmashauri ya Wilaya kama moja ya miradi iliyojumuishwa katika mpango wa Maendeleo wa Wilaya.

Wadau wengine muhimu ambao wanaweza kupendezewa na mradi huo wanaweza kuwa ni Wizara ya Elimu na Utamaduni, na ili kuhakikisha kwamba mradi unawiana na Sera ya Taifa ya Elimu, mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MEM) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MES). Wizara ya Fedha inaweza pia kuvutiwa na mradi huo.

Pia, ikiwa sehemu ya mradi huo imefadhiliwa na wahisani kutoka nje, ambapo ni lazima pawepo na makubaliano baina ya serikali ya Tanzania na Serikali ya nchi ya nje, kwa hiyo Wizara ya Katiba na Mambo ya Sheria husuan Mwanasheria Mkuu ni lazima awe ni sehemu ya mradi huo. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu watapenda kuhakikisha kwamba kati ya bajeti ya Serikali na rasilimali iliyokopwa inatumiwa kulingana na sheria. Mchakato huu ni muhimu katika utayarishaji wa muundo wa mradi katika ngazi zote.

### **2.2.3 Mfumo wa Kisheria**

Sehemu ya mradi hupima si tu mambo ya haraka ya kimkataba baina ya watendaji wa mradi, lakini pia ni kwa kiwango gani mradi husika unawiana na mkataba na makubaliano ya sheria ndogo za taifa na sheria za kimataifa. Maswala ya kisheria yatahusu mambo yote kama vile kutoa vielelezo, uanishaji bora na kiwango cha kodi kulingana na masharti yaliyopo. Maswala ya kisheria lazima yazingatie kanuni na taratibu zilizopo; kama vile viwango vya maji, sheria za majengo n.k

**2.3KIKAO 3: UZOEFU WA WASHIRIKI, MAJADILIANO NA MAFUNZO  
YALIYOPATIKANA**

<b>Madhumuni ya Kikao</b>
<b>Kubalishana uzoefu uliopita wa washiriki na kuhusisha uzoefu huo na somo la kikao cha 1 na 2</b>

Kikao hiki kitaangalia juu ya mambo mbalimbali na kazi za washiriki ukiwemo uzoefu wao, uhusiano na jumua zao na kila mmoja; stadi na maarifa wayapatayo ili kupata au kupanua huduma bora katika jumua zao.

Mojawapo ya jinsi ya kupata taarifa ni kuwataka washiriki kutoa maoni yao kwa kuwapa maswali ya kujaza ua kutoa maelezo kama ifuatavyo:

- a. Matumaini yako yalikuwa ni nini kuhusiana na mafunzo haya?  
Pamoja na hayo, yapi ni baadhi ya mafanikio ya uzoefu wako kwa jamii yako? Changamoto ni zipi? Kipindi cha 1 na 2 kimekusaidiaje katika mtazamo wako katika utayarishaji na ukadiriaji wa mradi?
- b. Je, umewahi kutumia mbinu ya uchambuzi shirikishi katika makundi ya jumua?
- c. Je, umeongoza au kusaidia mchakato wa kupanga mradi na watu katika jumua yako? Fafanua kwa kuelezea uzoefu huo.
- d. Je, utaainishaje stadi za kuandaa mradi wa Serikali ya Mtaa katika hatua hii kwa sasa? Stadi gani ya utayarishaji ungependa kuiendeleza?

### 3.0 MODULA 2: MCHAKATO WA MAANDALIZI YA MRADI

#### 3.1.1 Madhumuni ya jumla ya modula hii

Sehemu hii imebuniwa ili kuboresha mchakato wa upangaji na uteuzi wa mradi, mzunguko pamoja na kupata ufanisi unaotakiwa katika utekelezaji wake. Ni muhimu kutambua kwamba kuna umuhimu wa kupata stadi itakiwayo katika kusimamia miradi ambayo huja na mipango na maandalizi mazuri.

#### 3.1.2 Madhumuni ya mafunzo

Mwishoni mwa modula hii washiriki watakuwa na uwezo wa:-

- (i) Kutumia vigezo vya tathmini ya miradi na kufanya uchambuzi – kiuchumi, kiufundi, kijamii, kimazingira na kifedha.
- (ii) Kupitia hatua za mzunguko wa mradi na kujua mchakato ambao wanaweza kushirikisha jumuia.
- (iii) Kubuni mipango ya jinsi ya kutumia stadi na maarifa waliyopata katika kazi zao na kushirikisha stadi hizo kwa wengine.

### 3.2 KIKAO 1: UTAMBUAJI WA MRADI NA UCHAMBUZI YAKINIFU

<b>Madhumuni ya Kikao</b>
<b>• Kupanua tafsiri ya mradi</b>
<b>• Kueleza kwa washiriki namna mradi unavyofikiriwa na/au kutambuliwa</b>
<b>• Kupata dhana ya upembuzi yakinifu na uhusiano wake katika mchakato wa kufikiria na/au kutambua mradi</b>

#### 3.2.1 Hali ya Mradi na Utambuzi wake

Kwa nini na lini miradi inatambuliwa kuanzishwa hutegemea na Sera stadi na mashauriano ya wadau husika, mara nyingi Serikali. (Serikali kuu na za mitaa), AZISE au asasi za kimataifa, kwa mapana, kutegemea na madhumuni ya mradi na mikakati. Mitizamo miwili inaweza kutofautishwa kuhusu ni kwa jinsi gani miradi inaweza kutambuliwa katika Mamlaka ya Serikali za mitaa (LGA's). Ya kwanza ni ile ya mtizamo wa ki malengo. Hii ni miradi yenye mwelekeo wa kutoa huduma

zinazokusudiwa kwa walengwa. Ushiriki katika hali hii ni pale watu watakapoonyesha nia ya kushiriki katika shughuli zinazotakiwa.

Ya pili ni ile inayoweza kuitwa ‘ya kimchakato’. Hii ni katika shughuli maalum ambazo hutambuliwa na watu wenyewe. Utambuzi huu hufanyika katika misingi ya upatikanaji wa asilimali na mahitaji. Ushiriki katika hali hii ni watu wenyewe kutambua umiliki na uwajibikaji, katika shughuli ambazo wamezitambua na kuziendeleza kwa msaada wa mradi.

### **Utambuzi wa Mradi**

Mradi unaweza kutafsiriwa kwamba ni shughuli ya uwekezaji, ambapo rasilimali ya fedha imetumika kutengeneza rasilimali mtaji, ambayo itazalisha faida katika kipindi cha muda mrefu. Mradi huo unaweza kwa hiyo, kutazamwa kama kifurushi kilichotenganishwa cha uwekezaji, Sera, Taasisi na/au vitendo vingine vilivyotengenezwa ili kufikia madhumuni mahsusi ya kimaendeleo katika kipindi maalum cha muda, ikiwa na vitu vingi au mambo matano yafuatayo:

- i. Uwekezaji mtaji katika kazi za kiufundi, vifaa, au vyote (ambavyo huitwa matofali na zege ya mradi)
- ii. Utoaji wa huduma kwa usanifu na uhandisi, usimamiaji wa ujenzi, na uboreshaji wa shughuli na matengenezo.
- iii. Kuzipa nguvu asasi za kienyeji zinazojihusisha na utekelezaji na uendeshaji wa mradi, ikiwemo mafunzo ya mameneja na wafanyakazi wa ngazi za chini;
- iv. Maboresho katika sera kama vile katika kupanga bei, ruzuku, na kufidia gharama ambayo inaathiri ufanisi wa na mahusiano ya mradi kwa sekta, na madhumuni makuu ya maendeleo ya nchi.
- v. Mpango wa utekelezaji wa shughuli zilizotajwa hapo juu ili kufikia madhumuni ya mradi katika kipindi maalumu kilichopangwa.


Ili mradi uweze kufanikiwa vizuri, kanuni zake muhimu ni lazima zielezwe wazi. Nazo hujumuisha mambo yafuatayo:

- i. Madhumuni
- ii. Mazao tarajiwa
- iii. Wanufaika waliolengwa
- iv. Muda wa mpango
- v. Matokeo tarajiwa ya mradi

### **3.2.2 Ushirikishaji Asilia wa Utayarishaji Mradi**

**Mchoro 1: Ushirikishaji wa mazungumzo kuhusu mpango wa UPE ili kutambua miradi**

**inayofadhilika.**



Utambulishaji wa mradi ni lazima uwe kwa njia ya ushirikishaji, ukiwajumuisha jumuiya za kienyeji katika kuitambua na kuipa kipaumbele chake. Hivyo Serikali za chini za Mitaaa (Halmashauri za Wilaya na Manispaa) ni lazima zizingatie maoni ya wanajamii wakati wa kuchuja mapendekezo mbalimbali ya mradi na uteuzi wa mapendekezo yafaayo kwa ajili ya utekelezaji. Mchakato wa uchujaji ni lazima uzingatie na kujibu hoja zifuatazo:

- Je, teknolojia inasadifu na ina uhusiano na madhumuni ya mradi au uwezo wa wenyeji?

- Je, hatari zilizopo upo uwezekano wa kuzimudu?
- Je, mahitaji kwa ajili ya matokeo tarajiwa ni ya kuridhisha, na mradi kimsingi una faida za kufananishwa nazo?
- Je, usambazaji wa mali ghafi au stadi zake zinatoshesheza?
- Je, mpango katika makubaliano na uwezo wa taasisi na menejimenti unapatikana?
- Je, gharama zinazojirudia zinakidhi rasilimali za kifedha zinazopatikana?
- Je, kuna kuwajibika kwa kutosha kwa wanufaika walengwa na msaada kutoka katika mamlaka za Wilaya na Serikali Kuu?

Nafasi na vikwazo vya mbinu na mipango ya maendeleo, na ushirikishwaji wa uchanganuzi vijijini ni mifano miwili ya mwelekeo wa ushirikiwaji katika utayarishaji wa mradi. O & OD una sura zifuatazo:

- Ni mpango wenye mchakato kuanzia chini kwenda juu.
- Huanza kwa kuangalia fursa kuliko vikwazo ili kuwa na nia ya kutafuta suluhisho la vikwazo hivyo kwa maendeleo.
- Huendeshwa kwa muundo wa Mamlaka ya Serikali za mitaa na sambamba na mipango ya kitaifa na bajeti.
- Ni nguvu ya pamoja na huwezesha watu kupanga mipango yao kwa kutumia malengo katika NGPRS.

PRA kwa upande mwingine ni alama inayotolewa kwa makundi ya washirikishwaji kuhusu mbinu na mwelekeo unaotoa maarifa ya asili na kuwawezesha wadau kufanya uchanganuzi, uchambuzi na mipango yao. Kusudi la PRA ni kuwezesha wana maendeleo, maafisa wa Serikali pamoja kuanzisha, kujadili na kukuza mipango ya usimamizi.

PRA imegundulika kuwa na manufaa katika utayarishaji miradi kwa miaka mingi sasa.

### **3.2.3 Mfumo wa kimantiki kama zana ya kubainisha maeneo muhimu ya mradi.**

Mkakati wa Mfumo wa Kimantiki ni “Msaada katika kufikiri” sio kabadala cha uchambuzi ubunifu. Washiriki wanahamasishwa kuchota na kujaribia njia za ubunifu zitakazotumika katika mfumo fafanuzi. Mkakati wa mfumo wa kimantiki ni kifaa cha ufafanuzi, uwasilishaji na utawala ambacho kitawasaidia wanamipango na mameneja katika kuelewa mambo yafuatayo:-

- i. Kufafanua hali iliyopo wakati wa utayarishaji mradi
- ii. Kuanzisha mfumo wa utawala kidarajia (kingazi) ambao utarahisisha kufikiwa kwa malengo.
- iii. Kutambua hatari muhimu
- iv. Kuanzisha namna mazao na matokeo yake yatasimamiwa na kutathminiwa namna gani!
- v. Kuwasilisha muhtasari wa mradi katika viwango vinavyokubalika.
- vi. Simamia na kupitia miradi wakati wa utekelezaji.

Daima inatakiwa kutofautisha kati ya kile kiitwacho Mkakati wa Mfumo wa Kimantiki (LFA) na Chanzo cha Mfumo wa Kimantiki. Mchakato huhusisha uchambuzi wa tatizo, uchambuzi wa wadau, kufafanua darajia ya malengo, kuchagua mkakati mzuri wa kiutekelezaji. Kadhalika,

Matokeo ya mbinu hii ya uchambuzi ni kipimio kizuri ambacho hufupisha kusudio la mradi unaotarajiwa kufanywa na kwa namna gani. Yapi ni mawazo yaliyopo na mapato na matokeo yatasimamiwa na kutathminiwa namna gani.

Mkakati wa Mfumo wa Kimantiki unaweza kutumika katika kipindi chote cha mzunguko wa mradi katika maeneo yafuatayo:-

- i. Kutambua na kutathmini shughuli ambazo zinafaa katika kipindi chote cha mradi uliopendekezwa.
- ii. Kutayarisha mchoro wa mradi wenye mpangilio mzuri hatua kwa hatua na kimantiki.
- iii. Kukadiria ubunifu wa mradi

- iv. Kutekeleza mradi uliothibitishwa
- v. Kusimamia, kufanya mapitio na tathmini ya mchakato na utendekaji wa mradi.

Mkakati wa Mfumo wa Kimantiki unafaa uanze mapema katika mzunguko wa mradi, lakini chombo hicho cha kiuchambuzi kinaweza kutumika katika kusaidia kupitia na kuufanyia marekebisho ya kimuundo na katika mradi unaoendelea ambao hapo kabla haukutayarishwa kwa kutumia kanuni ya mkakati wa mfumo wa kimantiki. Mfumo huu (LFA) ni “Msaada katika kufikiri”, umetapakaa sana na unaweza kutumika popote.

**Jedwali 1: Jedwali** lifuatalo hapa chini linafafanua kwa ufupi mfumo wa kimantiki, ambao hutumika kwa kutumia kitu kimoja tu, alimradi msingi wa malengo, kwa kuangalia mambo muhimu ya mpango, ikiwa ni pamoja na malengo, madhumuni, na mazao tarajiwa na ni kwa namna gani shughuli hizo zimeshirikishwa na kuhusishwa na muundo wa Kitaasisi.

Malengo	Viashiria yamkini	Mbinu za kuthibitisha
Kuongeza uelewa wa na uwezo wa jamii kuelezea, njia za kienyeji za uchafuzi wa mazingira	Hatua za uelewa miongoni mwa makundi tofauti katika jamii (wanaume, wanawake, watoto) juu ya masuala mahsusi ya utunzaji na uchafuzi wa mazingira	Sampuli ya kutembelea shule, vikundi vya wanawake na wanaume wakuu wa kaya, kufanywa mwanzoni mwa mradi na baada ya miaka miwili. Itafanywa na maofisa wa utunzaji mazingira kwa kutumia dodoso kuangalia hatua za uelewa katika maeneo na masuala mahsusi.
	Kuanzishwa kwa kamati za kijamii zinazojihusisha na hifadhi na usimamiaji wa mazingira	Kumbukumbu za Wajumbe wa Kamati walioteuliwa, taratibu za vikao na kumbukumbu za maamuzi yaliyofanywa. Uchambuzi wa matokeo kila baada ya miezi sita dhidi ya vigezo vilivyoanzishwa na wajumbe wa kamati ya usimamiaji
	Uanachama, vikao na namba na aina ya shughuli zilizoanzishwa	Kutazama namna vikao vinavyoendeshwa, na kiwango cha ushiriki. Utendaji kazi wa maofisa wa hifadhi ya mazingira kulingana ratiba ya vikao iliyopangwa.



Istilahi za mkakati wa mfumo wa kimantiki

Zifuatazo ni baadhi ya istilahi muhimu zitumikazo katika mkakati wa mfumo wa kimantiki.

Maelezo ya Mradi hutoa muhtasari wa ni nini mradi utafanikishwa na kwa vipi. Hueleza njia ambazo zitatumika kufikia lengo.

**Lengo:** Huonyesha madhumuni kisekta au kitaifa, ambayo mradi utafanikisha k.m. kuongeza pato, ubora wa lishe au kupunguza uhalifu. Lengo, husaidia kuainisha kiwango cha ukubwa na ni mahali gani mradi unaingia/unafaa, na hueleza athari za muda mrefu ambazo mradi utachangia (japokuwa si lazima wenyewe kufikia lengo au kuwajibika kwa athari hizo).

Madhumuni ya Sehemu: Pale ambapo program ni kubwa kiasi, na ina sehemu nyingi (maeneo ya shughuli) ni vyema kuipa kila sehemu maelezo ya madhumuni. Maelezo haya ni laima yaonyeshe uhusiano kati ya matokeo ya sehemu na kusudio la mradi.

**Matokeo/Mazao:** Hii inahusu matokeo maalum na dhahiri ya mazao (vifaa na huduma) vinavyozalishwa kutokana na shughuli mbalimbali. K.m. inaweza kuwa ni pamoja na:- Mfumo wa umwagiliaji au upatikanaji wa maji, maeneo yaliyoendelezwa au kupandwa, watoto waliopata kinga, majengo na miundombinu mingine iliyoundwa, miongozo ya sera iliyotolewa, na idadi ya watumishi waliopewa mafunzo. Kila sehemu iwe na angalau zao moja, japokuwa inawezekana kuwa na manne au matano.

Utoaji wa mazao ya mradi kwa kiasi kikubwa unapaswa kuwa chini ya msimamizi wa mradi.

**Shughuli:** Hii inahusu kazi maalum zinazofanywa ili kufanikisha mazao hitajika. Mfano ni kama mpango mpya wa upatikanaji wa maji kwa jumuiia, ambapo inaweza ikaongezwa usanifu zaidi, uanzishwaji wa kamati za watumiaji wa maji, utaratibu wa ukarabati, maandalizi ya eneo (kiwanja), ukusanyaji wa vifaa asilia, ujenzi wa tanki na utandikaji wa mabomba, uchimbaji wa mashimo ya kunyonya na uzinduzi.

**Dhana/Hisia:** Hii inahusu hali ambayo inaweza kuathiri maendeleo au mafanikio ya mradi lakini ambayo mameneja hawana uwezo wa udhibiti wa moja kwa moja. K.m mabadiliko ya bei, mvua, sera za ardhi, na kutokutekelezwa kwa sheria zinazohusika. Dhana/Hisia ni maelezo chanya kwa sharti kwamba lazima yafikiwe ili mradi uweze kufanikiwa.

**Ishara/Dalili:** Hii inahusu taarifa zitakiwazo ili kusaidia kuamua maendeleo kuelekea kufanikiwa kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Ishara inapaswa, (ikiwezekana) kutoa tafsiri ya wazi kuhusu vipimo na malengo ikieleza kwa kina kuhusu kiasi, ubora, na muda wa matokeo tarajiwa.

**Namna ya kuthibitisha:**

Hii inapaswa kuweka wazi matarajio ya chimbuko la taarifa ambazo tunataka kukusanya. Tunapaswa kuangalia ni kwa vipi taarifa zitakusanywa (mbinu) nani atahusika na ni mara ngapi taarifa hizo zitakuwa zinatolewa.

### **3.2.4 Uchunguzi Yakinifu**

Uchunguzi yakinifu hufanywa ili kupata uhakika kwa ajili ya kujua ukubwa wa mradi na uwiano sahihi katika usanifu wa kiufundi, kiuchumi na upatikanaji wa fedha, vikwazo vya kimazingira

na kukubalika kwa kijamii; ikiwa ni pamoja na kukubalika kwake kisheria kulingana na malengo ya maendeleo ya Taifa, na kusadifu sera, sheria na mfumo wa kanuni. Lengo la uchunguzi yakinifu ni kwanza kubaini mambo yafuatayo:

- i. Malengo ya maendeleo dhidi ya makubaliano ya pendekezo la mradi;
- ii. Muundo wa sera na maelezo ya malengo ya mradi
- iii. Kukubalika kwa kiufundi kwa pendekezo;
- iv. Umakinifu wa usimamiaji wa mradi
- v. Hali ya mahitaji kwa ajili ya mazao ya mradi
- vi. Hali ya uchumi na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya pendekezo la mradi

- vii. Kuwafikiria wateja na utamaduni wa wanufaika wa mradi, na masuala ya kanuni.
- viii. Sera nyingine muhimu na matukio hatari (jinsia, mazingira, VVU/UKIMWI).

Matokeo ya uchunguzi yakinifu huathiri maamuzi kwa kupatikana au kutopatikana kwa rasilimali adimu kwa ajili ya mradi husika. Tathmini yakinifu kwa kawaida huweza kukwazwa na vitu asilia ambavyo sio sehemu ya maandalizi ya mradi.

Msingi wa maliasili katika Wilaya za Tanzania zipo katika mazingira ya ardhi, mali asili na watu. Harakati za kuhusisha maliasili hizi huhusisha uchaguzi katika matumizi ya ardhi na nguvukazi watu katika usuli wa matumizi ya ardhi asilia kwa watu wengi hususan huko vijijini ambako kuna elimu kidogo, athari hizi hukwamisha viwango vya uzalishaji katika wilaya hizo. Hali hii inadhihirika na dhamira ya Serikali ya kupambana nayo kwa kiwango cha hali ya juu dhidi ya umasikini uliotopea katika maeneo ya vijijini kwa kuanzisha sera nyingi, kwa mfano, Malengo – Mikakati ya Taifa ya kupunguza umasikini, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Tanzania (MMES).

Utekelezaji wa Sera hizi umetoa fursa ya kufanya uchaguzi kwa matarajio ya kutumia ardhi iliyopo, maliasili na rasilimali watu zilizopo.


### 3.3. KIKAO 2: MZUNGUKO WA MRADI KATIKA MUUNDO WA SERIKALI ZA MITAA

Malengo ya kikao
1. Kubaini hatua muhimu katika kuendeleza na kusimamia mradi na katika mchakato huo kupata sifa za mradi wenye mafanikio
2. Kutambua/kuona hatua za mzunguko wa mradi ambazo ni endelevu zenye uzito na zinazoweza kurudiwa.

#### 3.3.1 Makubaliano juu ya Muonekano wa Mzunguko wa Mradi

Washiriki watatakiwa kukubaliana juu ya mzunguko wa mradi na kisha kuainisha uzoefu wao katika miradi ya Serikali za Mitaa kwa kulinganisha na muundo wa mzunguko wa miradi.

Mchoro 2: Mzunguko wa Mradi



### **3.3.2 Hatua katika Mzunguko wa Mradi**

Kwa kawaida hatua za mzunguko wa mradi huonyeshwa kwa kutumia aidha mchoro wa mistari au mduara ukionyesha hatua za mradi kwa mfuatano.

-Ni mara chache miundo ya hatua za namna hii kuweza kuendelea achilia mbali kutekelezeka. Hatua kadhaa huweza kujitokeza kwa pamoja, na hivyo kusababisha utekelezaji/watekelezaji kurudi nyuma na kuangalia mambo fulani fulani.

Washiriki watachangia uzoefu wao katika mipango na utekelezaji wa miradi katika Serikali za mitaa (barabara na miundombinu, maji safi na taka, afya, elimu n.k) bila kujali ukubwa wa mradi.

Wakati wa kikao washiriki watapendekeza na kubaini sifa za miradi yenye mafanikio kulingana na mzunguko wa mradi utakavyokuwa unapitiwa upya.

Sifa za mradi wenye mafanikio ni pamoja na:-

- Kushirikisha jamii na wadau wengine wote katika hatua zote za kupanga mradi, utekelezaji na tathmini.
- Uchanganuzi wa hali halisi na kutambua ni nini hasa jamii inataka kufanya.
- Iwapo tatizo litagundulika uchanganuzi wa tatizo na kuchambua kiini kisha kufanyiwa kazi.
- Kukubali na kuwa na mwelekeo kuhusu masuala ya msingi kama umaskini, jinsia, utunzaji, mazingira n.k
- Yenye makusudio halisi na yanayowezekana
- Yenye malengo mazito
- Mradi uliochambuliwa na majukumu ya wahusika wote kuainishwa.
- Yenye mpangilio mzuri wa muda wa utekelezaji na bajeti kusudi malengo yake yaweze kutekelezwa katika muda uliopangwa kulingana na gharama.
- Utoe matokeo mazuri, yaliyowazi na thabiti wakati wa utekelezaji.
- Uwe na utaratibu mzuri wa usimamizi ili kupima maendeleo ya mradi.
- Ubaini matatizo na kutoa utaratibu wa jinsi ya kufanya mabadiliko ya lazima katika mradi.
- Mbinu za kuhakikisha kuwa jamii husika inakuwa na taarifa na inahusishwa katika mradi.

- Tathmini kwa kuzingatia maelekezo yaliyopangwa awali kwa kila hatua ya mradi na kisha mradi mzima baada ya kumalizika.
- Muundo wa mradi na mpangilio uliopangwa kimantiki.
- Watendaji wenye sifa waliopangiwa majukumu maalum.
- Mbinu za kufundisha wana jamii kuhusu matengenezo ya mradi iwapo utahitajika.

### 3.4 KIKAO 3: MCHANGANUO WA MRADI KIUFUNDI, KIUCHUMI, KIFEDHA, KIJAMII NA KIMAZINGIRA

Malengo ya kikao
• Kuelezea uchanganuzi wa masuala ya kiufundi katika mradi
• Kuelezea uchanganuzi wa masuala ya fedha katika mradi
• Kuelezea uchanganuzi wa masuala ya kiuchumi katika mradi
• Kuelezea uchanganuzi wa masuala ya mazingira katika mradi
• Kuelezea masuala ya kijamii katika mradi

#### 3.4.1 Ukadiriaji wa Ukubwa wa Mradi

Kama inavyotegemewa, wakati wa tathmini ya ukubwa wa mradi maswali mazito yataulizwa na majibu yake ndiyo yatakayotoa picha iwapo pendekezo la mradi litakubaliwa au kukataliwa. Maswali yatakayoulizwa yatahusu kufaa kwa malengo ya mradi, ukubwa, uwezo, mbinu za utekelezaji na namna yake, muda wa utekelezaji pamoja na masuala ya kiufundi, kifedha, kiuchumi, kisiasa, kimazingira, kijamii na uwiano wa usambazaji wa mradi

#### Uchanganuzi wa Kiufundi

Uchanganuzi wa kiufundi kwenye mradi, unakusudia kuthibitisha yafuatayo:

- i. Kuthibitisha chimbuko la pendekezo la mradi, hali ya uchunguzi ikiwa ni pamoja na tathmini na uchunguzi uliofanyika kabla ya kutoa pendekezo na hali ya maamuzi yaliyochukuliwa na mamlaka husika zilizoshirikishwa.
- ii. Kwamba tatizo au mahitaji yanayohitaji utatuzi kutokana na mradi yameelezwa waziwazi.
- iii. Kwamba mradi umeelezwa kwa uwazi kwa upande wa masuala ya kiufundi (kama ukubwa, mahali, muda na teknolojia)

- iv. Kwamba vifaa vinavyohitajika vimefafanuliwa na upatikanaji wake umebainishwa.
- v. Kwanza gharama za mradi zimeelezewa, matarajio ya bei za bidhaa zimeainishwa na utaratibu wa malipo na ratiba umekubaliwa.

### **Uchanganuzi wa Kiuchumi**

Haja ya uchanganuzi wa kiuchumi unajitokeza kutokana na sababu kwamba Serikali za Mitaa wana rasilimali finyu kuweza kujiendesha. Kutokana na rasilimali finyu kunakuwa na ugumu wa uamuzi wa kuchagua ni wapi rasilimali hizo zipelekwe kwa vile kunakuwa na miradi mingi inayopewa kipaumbele na uamuzi hauna budi kufanywa na maafisa wa Serikali za Mitaa.

Gharama za kiuchumi na manufaa ya mradi hukadiriwa kwa kutumia uchanganuzi wa gharama, manufaa ya mradi ambayo huainisha tathmini ya gharama za kijamii ambazo hazitajwi, na zile zinazotoka nje ya mradi. Kwa miradi inayozaa faida, mambo yanayotathminiwa upatikanaji wa faida kama thamani ya sasa, mapato ya ndani, muda wa kulipa na nyongeza ya faida, hutumika kutathmini na kukadiria ubora wa mradi

Kwa kawaida Serikali za Mitaa huwa hawaweki suala la faida mbele wakati wa kufikiria miradi. Hivyo suala la manufaa ya mradi kwa jamii ndilo jambo linalopewa kipaumbele. Katika uchanganuzi wa gharama za manufaa kwa jamii mtu anaweza akauliza maswali ya msingi kama ni kwa gharama na manufaa gani ya moja kwa moja na yasiyo ya moja kwa moja ambayo wanufaika watapata kwa upande wa kupunguza umaskini, kuongeza pato, kuboresha huduma za matibabu, elimu, maji na huduma za afya.

### **Uchanganuzi Gharama - Faida**

Mahali ambapo uchanganuzi wa ki-uchumi unahusika na kuonyesha thamani ya athari za kimazingira zitokanazo na shughuli za mradi, uchanganuzi wa Gharama Faida ni muhimu. Hii huusisha mlolongo mzima wa faida na gharama katika shughuli kulinganisha hizi kwa kutimbia bei zilizopo, na kisha kupata athari halisi za shughuli/tendo.

Linalojitokeza katika uchanganuzi wa gharama faida, ni madhumuni ya kuonyesha kiwango cha mwisho cha faida za kiuchumi kutokana na taswira ya ustawi wa binadamu.

Hata hivyo uchanganuzi wa Gharama Faida huitaji taarifa za kina kuhusu athari zinazoweza kupimwa, na huusika hasa na masuala ya ubora wa uchumi unaohusishwa na siyo masuala mengine yanayoweza kuhusiana na watoa maamuzi. Uchanganuzi bora wa Gharama Faida ni ule unaoonyesha mashaka na kujali usambazaji, lakini haina uwezo wa kushughulikia madhumuni yenye sehemu nyingi. K.m mahitaji ya taarifa kwa uchanganuzi wa Gharama Faida yanaweza kupatikana kupitia EIA na EA kwa sababu takwimu halisi huchuku sehemu kubwa katika mradi.

### **Uchanganuzi wa Gharama zenye Matokeo Tarajiwa.**

Uchanganuzi wa Gharama zenye Matokeo Tarajiwa unaweza kuwa bora kuliko uchanganuzi wa Gharama Faida ambapo upimaji wa faida ni mgumu.

Badala yake upimaji wa faida kwa lengo unaanzishwa, na njia za chini za kufikia kiwango cha faida kinatathminiwa. K.m. inaweza ikawa vigumu kukadiria na kulinganisha faida za Misititu, na kuweza kupima na kuteua maeneo ya asili ndani ya eneo la Halmashauri. Kwa kutumia uchanganuzi wa Gharama wenye Matokeo Tarajiwa unapata angalau eneo linaloweza kuhifadhiwa, kukadiria Gharama za kulinda maeneo yote yanayowezekana, na kwa kulinganisha Gharama hizi, kuweza kuteua ni maeneo gani yanahitajika na yenye Gharama nafuu zaidi.

Mchoro 3 : unaelezea mchakato mzima wa maandalizi ukijumuisha hasa wanufaika wa matibabu, maji safi na taka katika kujadiliana juu ya kuunda mradi. Mchakato wa maandalizi, huruhusu mawazo zaidi kuingizwa kwenye mradi na mara nyingi husaidia kufanikisha mradi.



### MCHORO 3: Mpango Shirikishi




#### Uchanganuzi wa Fedha

Uchanganuzi wa masuala ya fedha huchukua mtazamo mzito kwenye vyanzo vya upatikanaji wa fedha. Hii ni pamoja na masuala ya umaliziaji wa mradi na uendeshaji endelevu. Hivyo uchanganuzi lazima uhoji:

- i. Iwapo Serikali ya Mtaa itatekeleza mradi kutokana na mapato ya ndani?
- ii. Iwapo Serikali ya Mtaa itatekeleza mradi kutokana na mapato toka nje?
- iii. Je, mapato ya nje itakuwa ni fedha ya mkopo?
- iv. Iwapo fedha zitakuwa ni za mkopo, je, Serikali ya Mtaa itakuwa na uwezo wa kulipa pamoja na riba?
- v. Je, mapato ya nje yatakuwa ni ruzuku kutoka Serikali Kuu au sehemu nyingine?
- vi. Je, Serikali ya mtaa inaweza kugharamia mradi kwa kushirikiana na mfadhili wa nje awe ni Serikali kuu au mshirika mwingine wa maendeleo.
- vii. Je, Kutakuwa na utaratibu wa kufidia gharama za mradi utakaowekwa?
- viii. Kutakuwa na utaratibu wa usimamizi wa fedha kwa kuweka kumbukumbu za fedha wakati wa utekelezaji na uendeshaji wa mradi?

Nyaraka za kumbukumbu ni daftari za fedha, kumbukumbu za mali, taarifa za benki, mizania, mchanganuo wa mapato, mtiririko wa fedha,(utaratibu wa mapokezi na malipo n.k mchoro Na. 4 hapa chini unaonyesha kamati ikiwa kazini ikishughulikia bajeti ya fedha.

#### **MCHORO 4: Kipindi cha Bajeti ya Fedha ya Wilaya**



#### **Uchanganuzi kuhusu Mambo ya Mazingira**

Kutegemea na hali ya mradi, ni muhimu kwamba mradi uendane na masharti yaliyowekwa na NEMC. Hasa mradi uwe katika matakwa ya kisheria. Masuala ya kimazingira ambayo mradi unapaswa kujishughulisha nayo ni:-

- Afya ya jamii na usalama wa shughuli zao.
- Udhibiti wa hewa, maji na uchafuzi wa ardhi.
- Usimamizi wa ubadilishaji maliasili (mimea na wanyama)
- Matumizi bora ya maliasili kwa njia mbalimbali, mzunguko na udhibiti wa mmomonyoko.
- Utunzaji wa viumbe pekee (misitu na mbuga za wanyama kwa ajili ya uhifadhi wa utamaduni)
- Suala hili la kujali mazingira linashughulikiwa zaidi kama kifungu tofauti katika kipimo 3.

## **MCHORO NA. 5: Unaonesha uchafuzi na mazingira**



### **Uchanganuzi wa Kijamii**


Uhalali wa dhahania ya mradi kuhusu hali ya kijamii hupimwa kwa kupitia uchanganuzi wa kijamii na iwapo ni lazima marekebisho yanaweza kufanywa ili malengo ya mradi yafafanuliwe na kutoa maana zaidi kwa umma pamoja na asasi za utekelezaji.

Uchanganuzi wa kijamii huelekezwa katika maeneo manne kama ifuatavyo:

- i. Utamaduni jamii na tabia ya kuweka takwimu za vizazi, vifo, maradhi katika jamii inayohusika na mradi. Ukubwa wa umma, muundo wa kijamii hii ikiwa ni pamoja na maadili, jinsia, umri na tabaka
- ii. Ni kwa namna gani Umma wa mradi umejipanga ili kuendesha shughuli za uzalishaji ikiwa ni pamoja na muundo wa kaya na familia, upatikanaji wa wafanyakazi, umiliki wa ardhi, pamoja na upatikanaji na udhibiti wa rasilimali.
- iii. Ukubalikaji wa mradi kiutamaduni, kwa maneno mengine uwezo wake wa kurekebisha na kuleta mabadiliko tarajiwa katika tabia za watu na jinsi wanavyotambua mahitaji yao.

- iv. Mkakati muhimu wa kushawishi uwajibikaji kutoka umma wa mradi na kuhakikisha ushiriki endelevu kuanzia kupanga hadi mafanikio ya utekelezaji, uendeshaji na ukarabati

#### **MCHORO 6 – Unaonyesha Jinsia (mtoto wa kike) anavyopuuzwa**



#### **Matukio Hatari:**

Kanuni zilizotajwa hapo juu kuhusu uchanganuzi wa kijamii zina uwezo sawa katika kutathmini athari za matukio hatari kama VVU/UKIMWI, mazingira na masuala ya jinsia ili kupima ubora wa mradi. Hii hasa ni pale ambapo gharama na manufaa yasiyo dhahiri yadhaniwayo ni kutokana na matukio hatari. Hivyo yanatiliwa maanani wakati wa makadirio ya jumla ya mradi unaopendekezwa.

#### **MCHORO 7: Unaonyesha hali halisi ya umaskini**



#### **4.0 KIPIMO 3: UKADIRIAJI WA ATHARI ZA MAZINGIRA NA SERA ZA HIFADHI**

##### 4.1.1 Malengo ya jumla ya kipimo hiki.

Kipimo hiki kinataka kuonyesha utambuzi wa wahusika wa Serikali za Mitaa kuhusu mchakato wa tathmini ya athari za mazingira ambazo zinaunganisha mazingira, uchumi na malengo ya kijamii katika uamuzi kuhusu mradi.

##### 4.1.2 Madhumuni ya mafunzo

Mwishoni mwa modula hii, washiriki wataweza:-

- (i) Kuendeleza uwezo wa kuunganisha masuala ya mazingira katika mzunguko wa mradi.
- (ii) Wamejifunza misingi, taratibu na mazoezi ya uunganishaji wa masuala ya mazingira kupitia EAI
- (iii) Kuwa na uelewa juu ya masuala ya kisheria katika uunganishaji wa masuala ya azingira katika kupanga miradi, kusanifu, tathmini, usimamizi na uthamini.
- (iv) Kuwa na uwezo wa kutafuta na kupata ushirikishwaji wa UMMA katika EIA na kuunganisha masuala ya kijamii na kiuchumi katika mzunguko wa mradi.
- (v) Kuanzisha mpango wa jinsi ya kutumia stadi na maarifa waliyojifunza kwenye kazi zao pamoja na kuwashirikisha wengine.

## **4.2 KIKAO 1: Mtazamo juu ya Mazingira na “Tathmini ya Athari za Mazingira na Sera ya Hifadhi”**

4.2.1 Tafsiri ya neno ‘Mazingira’: Ili kuweza kuwa na utambuzi juu ya “Tathmini ya Athari za Mazingira na Sera ya Hifadhi” washiriki hawana budi kuelewa maana ya neno “Mazingira”. Hii ni muhimu kwa sababu washiriki ni watu wanaotoka maeneo na mazingira tofauti hivyo kutokuwa rahisi kwa kila mmoja kupata (kuelewa) dhana ya neno hilo. Mazingira humaanisha maumbile ya mahali yanayomzunguka binadamu ambayo ni pamoja na ardhi, maji, anga, hewa, sauti, radha, na mambo mengine ya kibailojia kuhusu mimea, wanyama, mambo mengine ya kijamii ambayo aidha ni asili au yamejengwa, (DANIDA – 2001).

### 4.2.2 Mfumo wa Sera na Sheria kuhusu Usimamizi wa mazingira

Utekelezaji wa miradi na Mamlaka ya Serikali za mitaa lazima ufanywe kulingana na maelekezo ya Sera ya Taifa ya mazingira (NEP) ya mwaka 1997 na Sera ya Taifa ya ardhi ya mwaka 1995.

pia sheria Halmashauri ya Taifa ya usimamizi wa mazingira (No. 9 ya mwaka 1983), ambayo kimsingi ndiyo iliyoruhusu uanzishwaji wa Halmashauri ya Taifa ya usimamizi wa mazingira (NEMC). Pamoja na mambo mengine, sheria inafafanua shughuli na majukumu ya NEMC.

Pia sheria za ardhi No. 4 na 5 za mwaka 1999. Hizi hufanya uwezekano mdogo wa kufikiwa kwa sheria za usimamizi wa mazingira na maliasiali kwa sababu zinatoa tafauti kwa ardhi katika sehemu tatu:

1. Ardhi ya jumla (Isiyo na hifadhi au ardhi ya Umma)
2. Iliyohifadhiwa (Inayolindwa)
3. Ardhi ya Kijiji (ardhi ambayo iko ndani ya mamlaka ya Serikali ya kijiji tofauti na ile inayomilikiwa na Serikali kuu).

Mwisho Sheria ya Serikali za Mita (Halmashauri ya Wilaya ya mwaka 1982 sehemu III kifungu kidogo cha 2 (c) inatoa majukumu kwenye Mamlaka ya Serikali za mitaa kuhifadhi mazingira. Matokeo yake kila Halmashauri ya Wilaya ina Kamati maalum ya mazingira ikiwa na majukumu maalum.

### **Mazingira na Sera ya Hifadhi Jamii.**

Uhifadhi wa mazingira na makazi ya asili ni muhimu katika upangaji wa maendeleo ya muda mrefu. Miradi ambayo inahusisha kubadilisha maeneo ya makazi asilia inapaswa kukataliwa, labda kama hakuna njia mbadala, na iwapo uchambuzi utaonyesha kuwa faida ya jumla kutoka kwenye mradi inazidi Gharama za Mazingira.

Iwapo kutokana na utekelezaji wa mradi, watu wataathirika kwa kupoteza ardhi, mali, pamoja na kupoteza uwezo wa kuzifikia rasilimali zao, sera ya kuhamishiwa/kuhamia makazi mapya inaweza kutumika. Kwa ajili hii, Serikali ya Tanzania imeandaa mfumo wa Sera ya kuhamishiwa/kuhamia makazi mapya ambayo inaelezea utaratibu wa kuhamia/kuhamishiwa makazi mapya pamoja na fidia, inayopaswa kufuatwa iwapo ukariaji wa kimazingira umeonyesha kuwa watu wataathiriwa na shughuli za mradi.

Athari zinazotokana na kuhamishwa bila ridhaa ili kupisha miradi ya maendeleo inaweza kuathiri wahusika kwa:-

Matatizo ya ki uchumi kijamii na kimazingira ambapo uzalishaji unavurugwa, watu kuwa na umaskini wa kipato kutokana na kupoteza uwezo wa uzalishaji, vitendea kazi na rasilimali. Watu

kupelekwa maeneo ambayo hayasitawishi au stadi zao za uzalishaji hazitumiki, na kugombania rasilimali zilizopo. Koo mbalimbali kutenganishwa, na hivyo mila na desturi kupotea.


Sera ya kuhamishwa inaweza kutumika kwa sababu mradi husika unaweza kuhitaji ardhi. K.m Sehemu ya ardhi inatakiwa, na kuna watu wanaitumia kwa kilimo na/au wamejenga nyumba sehemu ile, au wanaweza kutumia ardhi hiyo kwa umwagiliaji na malisho ya mifugo, au kuitumia katika masuala ya ki uchumi, kiimani au vinginevyo, ambapo shughuli hizo haziwezi kuendelea wakati na baada ya utekelezaji wa mradi. Kwa hali hiyo watu hao itabidi wafidiwe mali zao (ardhi na mali nyingine). Hii inaweza ikawa ni kwa pesa au kwa mali kulingana na mdai anavyopendelea.

Sheria Na. 4 pamoja na sheria ya vijiji Na 5 ya mwaka 1999 zinatoa utaratibu wa wazi wa ufidiaji inapochukuliwa ardhi kutoka kwa raia (Mwananchi).



Taratibu hizi ni lazima zizingatiwe hasa zile za ardhi (taratibu za ukadiriaji wa thamani na fidia) ambazo zimewekwa chini ya S 179 ya sheria ya ardhi Na 4 ya 1999. Taarifa ya serikali (GN Na. 78 iliyochapishwa 4/5/2001)

#### 4.2.3 Mchoro Na. 8: Aina 3 za vipimo vya ukubwa wa mazingira –



Kipimo cha ekolojia huchanganya mimea na wanyama na mfumo wa ekolojia, wakati kipimo cha uchumi jamii ni yale mazingira yaliyojengwa ikiwa ni pamoja na miundo mbinu. Kipimo utamaduni jamii, ni masuala ya kijamii na kiutamaduni. Inapaswa ieleweke kuwa vipimo hivi vitatu siyo kwamba vinaishi kama vitu vinavyotegemeana bali vinavyohusiana. Ni muhimu kwa washiriki kutambua masuala ya mazingira kwa mtazamo huo.

#### 4.2.4 Utambulisho kuhusu Athari za Mazingira na Mahitaji yake:

Kabla ya kuelezea maana ya –Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA), ni muhimu washiriki wakaainisha mtazamo wao kwamba EIA ni nini kwao. Ni bora kuwa na utambuzi wa EIA na kuondoa kabisa masuala ambayo ni ya upotoshaji kuhusu EIA.

Manufaa ya EIA ni pamoja na:-

- i. EIA ni chombo muhimu cha msaada katika kuchanganua na kuteua miradi bora ya mazingira
- ii. EIA hufanikisha utoaji wa maamuzi yaliyoboreshwa
- iii. EIA husaidia na kuhakikisha upangaji wa miradi endelevu na utekelezaji wake.

- iv. EIA hutumika kutambua uboreshaji ili kuzuia madhara zaidi ya mazingira.
- v. EIA inaweza kwa kiwango kikubwa kusaidia kuzuia hatua za urekebishaji zenye gharama.

### **EIA ni nini?**

EIA ni mfumo wa kupata na kutathmini taarifa za mazingira kabla ya kuzitumia katika utoaji maamuzi na mchakato wa maendeleo. Taarifa hizi kimsingi huwa utabiri wa jinsi gani mazingira yatakavyoweza kubadilika iwapo mambo fulani fulani yatatekelezwa na ushauri wa ni kwa namna gani usimamizi wa mazingira unaweza kuteuliwa na kutekelezwa. Hadi siku za karibuni EIA imekuwa ikijielekeza kwenye maendeleo ya maeneo ya ujenzi kama barabara kuu, vituo vya umeme, miradi ya maji, na viwanda vikubwa.

Taratibu lakini kwa wingi, miradi imepanuka na kuhusisha sera, mipango na shughuli nyingine ambazo ni sehemu ya mchakato wa maendeleo.

Watoa maamuzi hupewa na EIA, taarifa na (mara nyingi mapendekezo) kuhusu matokeo ya maamuzi yao.

Kusudi muhimu la EIA ni kuanzisha mfumo madhubuti wa kujali masuala ya mazingira katika sehemu zote muhimu za utoaji maamuzi kwa miradi maalum ya shughuli za maendeleo.

Washiriki wanapaswa kuelewa kuwa wajibu wa EIA ni kuhakikisha kuwa mazingira ni moja ya vipengele ambavyo vinaangaliwa wakati wa kutoa maamuzi.

### **EIA Katika Mzunguko wa Mradi**

Kutokana na umuhimu wa EIA kama chombo cha mipango, na kwa kuwa wengi bado wanatumia mikabala ya asili katika kupanga mipango na hivyo kujikita zaidi kwenye masuala mengine ya ki-uchumi kuliko mazingira, ni vyema washiriki wakafahamishwa kuhusu mbinu za

kuiingiza EIA katika mzunguko wa mradi ili kuifanya EIA sehemu ya mchakato mzima wa mipango.

#### **4.2.5 Tathmini ya Athari: Chimbuko na umuhimu wake**

Mojawapo ya mambo muhimu ya kiufundi katika EIA ni uwezo wa kutambua, kuchambua

na kutathmini athari zinazoweza kutokana na mazingira kutokana na mapendekezo ya mradi wa maendeleo ikiwa ni pamoja na kutambua chimbuko la athari hizo. Washiriki wanahitaji kuwa na maoni juu ya mbinu za kutambua athari, chimbuko lake na sababu. Maswali ya msingi ya kuuliza wakati wa tathmini ya athari za mazingira ni pamoja na:-

- i. Ni nini kinachosaidia kukamilisha mradi au shughuli iliyopendekezwa?
- ii. Ni nini kinaweza kutokea kwa mazingira kutokana na mradi husika?
- iii. Ni kwa kiasi gani matokeo hayo yatakuwa?
- iv. Je matokeo hayo yataathiri sana?
- v. Kama ndivyo, nini kifanyike kupunguza mabadiliko?
- vi. Ni kwa vipi mabadiliko yanayoonekana na shughuli za kupunguza athari hasi yanaweza kutumika kwa ajili ya utoaji wa maamuzi?

Vigezo vya kuamua umuhimu wa athari ni pamoja na:-

- i. Umuhimu wa ekolojia
- ii. Umuhimu wa kijamii
- iii. Umuhimu wa kiuchumi
- iv. Viwango vya kimazingira (Kitaifa na Kimataifa)
- v. Vipengele chanya na hasi

**Vipengele Maalum vya Kutathmini Umuhimu wa Athari ni pamoja na:-**

- Kiwango cha athari kwa wananchi (umuhimu kwenye jamii)
- Hii ni pamoja na uwezekano wa athari kwa afya ya binadamu.
- Uwezekano wa kupoteza ardhi ya kilimo
- Kupoteza uzuri na thamani ya maumbile
- Ushindani na mahitaji juu ya rasilimali za umma
- Athari za demografia (taaluma za kitakwimu)
- Mahitaji juu ya miundo mbinu na huduma nyingine

- Mtizamo hasi juu ya thamani na maisha ya jamii

### **Maamuzi ya Kitaalamu na Kisayansi**

Hii ni pamoja na maoni ya kitaalamu katika fani husika

Ulinganifu wa viwango vya mazingira, hii ni pamoja na majukumu ya kitaifa na kimataifa juu ya uhifadhi wa uasili na mazingira.

#### **4.2.6 Hatua za Kupunguza Makali**

Mbali na kutambua athari na chimbuko lake, wajibu wa msingi wa EIA ni uwezo wa kutoa huduma za kupunguza makali kwenye athari zinazotambuliwa. Washiriki wanapashwa kujitahidi kuisisitiza juu ya kusudi la umuhimu wa kupunguza makali. Hii ni pamoja na:-

- i. Kutafuta njia bora za kutekeleza mambo.
- ii. Kupunguza au kuondoa kabisa mitizamo hasi.
- iii. Kuimarisha manufaa ya mradi
- iv. Kulinda haki za wananchi kuhusu fidia.

Mipango bora ya upunguzaji makali ina sifa zifuatazo:-

- i. Kudhibiti hatua za kuzuia, kuondoa au kupunguza athari
- ii. Kuongeza shughuli zinazohitajika za kutekeleza miradi
- iii. Kutambua wahusika, ikiwa ni pamoja na majukumu ya ki-asasi katika kutekeleza hatua za kupunguza makali.
- iv. Kutoa taarifa za kiufundi kuhusu hatua za kupunguza makali.
- v. Kutambua na kupanga ratiba ya kuelimisha juu ya baadhi ya vipengele vya mpango wa upunguzaji makali.
- vi. Kutambua taratibu za usimamizi na utoaji taarifa pamoja na rasilimali zinazotakiwa kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa upunguzaji makali.

#### **4.2.7 Wajibu wa Washikadau Katika Usimamizi wa Mazingira na Mapitio ya Ukadiriaji wa Athari za Mazingira (EIA).**

Uzoefu wa EIA ki ulimwengu, unaonyesha kuwa uhusikaji wa washikadau na hivyo kuongeza ushirikishwaji ni mchango muhimu katika mpango mzima wa EIA, kuhusu taarifa na utoaji maamuzi.

Uhusishwaji wenye ukomo hasa kwa wana jamii ambao wako katika mwelekeo wa kiathiriwa na mradi mara nyingi husababisha matatizo ya kisiasa na manunguniko huelezwa mwishoni mwa utafiti wa mradi. Matokeo haya huweza kuongeza kazi kutegemea na uzito wa maoni na wakati mwingine kwenda mahakamani na kuchelewesha utekelezaji, hivyo kusababisha ongezeko la gharama za mradi.

Wakati wa mawasiliano na EIA washiriki wanapaswa kuelewa ni vipi ushiriki wa wana jamii na wadau unavyoweza kufanikiwa. Washiriki wataelekezwa kuhusu taratibu tofauti na ni jinsi gani zinavyotumika.

Mbinu za ukusanyaji wa takwimu na jinsi ya kuhamasisha wana jamii itajitokeza. Washiriki watapanga mikakati ya namna ya kuihusisha jamii katika masuala ya EIA ambayo wanayaendesha au wana mkataba. Washiriki pia watapewa nafasi ya kujadiliana juu ya uzoefu wao kuhusu ushirikishwaji umma katika EIA.

Ushirikishwaji wa washikadau husaidia kuhakikisha kuwa hadhi ya EIA inadumishwa katika kiwango cha juu kinachokubalika. Kimsingi kwa kupitia ushirikishwaji wa washikadau kuna utaratibu wa wazi ambapo matokeo ya awali na rasimu ya EIA inaweza kutumika kubadilisha/kurekebisha mradi ili kuuboresha zaidi

Masuala ya uwiano wa utoaji maamuzi yanapashwa kujengwa katika EIA. Hii ni pamoja na:-

- Kuwe na utaratibu unaotambulika wa kupitia upya na taratibu za mashauriano zitakazoshirikisha washikadau wengi kwa kadri iwezekanavyo.
- Haki ya kukata rufaa kwa yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi na
- Kuweka wazi maamuzi na sababu zote mbele ya wananchi.

## **5.0 MODULA 4: UCHUNGUZI – KIFANI KUHUSU UCHANGANUZI WA MRADI NA TATHMINI YA MAFUNZO**

### **5.1.1 Malengo ya jumla ya Modula:**

Kipimo hiki kinakusudia kuwafanya washiriki kwa mwingiliano kutumia maarifa na ujuzi

walioupata katika kutatua matatizo ya kimaisha kuhusu tathmini ya mradi.

### **5.2 KIKAO 1 – UCHANGANUZI WA MRADI**

<b>Malengo ya kikao</b>
<b>Kwa washiriki kuweza kutumia maarifa waliyoyapata kwa ajili ya kuimarisha tathmini ya mradi – uimara na uchunguzi kifani.</b>

### **5.3 KIKAO 2: MAPITIO YA MAFUNZO YA SIKU 1, 2,3 NA 4**

<b>Malengo ya kikao</b>
<b>Kupitia masomo yote waliyojifunza siku 1,2,3,na 4</b>

### **5.4 KIKAO: TATHMINI YA MAFUNZO**

<b>Malengo ya kikao</b>
<b>Kuelezea umuhimu na matumizi ya mbinu za tathmini baada ya mafunzo na wakati wa kazi, na washiriki kujadili njia za kutumia ujuzi mpya wawapo sehemu zao za kazi.</b>

#### **4.0 KIAMBATISHO 1: FAHARASA**

##### **Tathmini**

Ukadiriaji kulingana na vigezo vilivyowekwa kwa ajili ya kutoa maamuzi kuhusu uchunguzi yakinifu, ukubalifu wa mradi au programu yake kabla ya kuingia kwenye utoaji wa fedha. Vigezo huwa ni pamoja na mahusiano na uendelevu. Tathmini inaweza pia kuhusisha uchambuzi wa maoni kama sehemu ya mchakato wa uteuzi wa mradi wa kupewa fedha.

##### **Tathmini ya Kiufundi**

Hii huwezesha mchakato wa tathmini kufanyika kwa utaratibu mahsusi wa hali muhimu ya mradi – kimazingira, kimaumbile, kijamii, kifedha, kiuchumi, kiutamaduni, kisiasa, kiutawala, na kitaasisi iliyopo katika eneo ambalo uwekezaji unaenda kufanywa.

##### **Takwimu za Msingi**

Taarifa iliyokusanywa katika sekta maalum na katika eneo maalum la kijiografia, ambayo itachanganuliwa ili kuwezesha kudhihirisha usahihi wa mradi huo kuingia katika sekta hiyo na mahali hapo.

##### **Mahitaji ya Jamii**

Matakwa halisi, mawazo na mahitaji muhimu, mahitaji na matamania ya jamii, ambayo kwa kawaida huunda msingi wa kuunda na kutathmini mipango ya maendeleo ya jamii.

##### **Gharama matokeo tarajiwa**

Ni mlinganisho wa gharama za kufikia lengo au mazao kwa njia tofauti. (hutumika pale ambapo faida ni ngumu kuamuliwa)

##### **Mchanganuo wa Gharama – Faida**

Hii hujumuisha seti ya kiufundi kwa kulinganisha mpango wa uwekezaji mbadala au miradi ambayo inatarajiwa kutoa mazao yenye faida kwa miaka mingi.

##### **Athari Limbiko:**

Ni athari zitokanazo na athari za nyongeza za kazi zilizoongezeka katika mpango kazi kwenye athari za matendo mengine yaliyopita, yaliyopo na yajayo.

##### **Mwendelezaji**

Mtu, kundi la watu au wakala wa kuendeleza mradi ambao ni maalum katika mchakato wa tathmini ya athari ya kimazingira.

##### **Athari ya Moja kwa Moja**

Athari ambazo zinasababishwa na tendo na ambayo kwa kawaida hutokea katika wakati na mahali hapo hapo kama tendo.

### **Mchanganuo wa Kiuchumi**

Huu huzingatia fursa za gharama ya uwekezaji mbadala katika ukadiriaji wa faida ya mradi husika unaofikiwa

### **Thamani ya Kiuchumi**

Thamani ya mradi uliopimwa katika mawanda kama uwezo wake wa kutengeneza ajira na mapato, kuongeza usafirishaji nje wa bidhaa na kuongeza kodi ya mapato.

### **Ubona na Matokeo**

Ni namna mradi unavyoweza kufikia madhumuni na malengo yake k.m ni mambo gani ya kimaendeleo ambayo yamefikiwa au yanatarajiwa kufikiwa.

### **Kufaa**

Kiasi ambacho madhumuni ya mradi yamefanikishwa au yanatarajiwa kufanikishwa kwa kutilia maanani umuhimu wake.

### **Ufanisi**

Kipimo cha namna zana za kiuchumi (fedha, utaalumu, muda n.k) zinavyoingai katika mazao

### **Mfumo wa kimantiki wa Matriki**

Ni chati yenye vyumba vine na mistari minne ambayo hutoa muhtasari wa nini mradi umakusudia kufanya na kwa vipi (zama muhimu, mazao, kusudi na madhumuni) suala muhimu ni kwa vipi mazao na matokeo vitasimamiwa na kutathminiwa.

### **Umuhimu/Maana**

Tathmini ya kitaalamu/maamuzi juu ya kiwango cha athari kwa mazingira iwapo mradi utatekelezwa. Hii ina maana ya kusababisha mabadiliko katika mazingira ya asili yanayomzunguka binadamu k.m ardhi, maji, anga, hali ya nchi sauti, harufu, ladha, masuala ya kibailoia k.v wanyama na mimea. Masuala mengine ya kijamii ambayo aidha ni asili au yamejengwa.

### **Mazingira**

Athari za kimaumbile za mazingira ya binadamu yakiwemo ardhi, maji, anga hewa, hali ya hewa, sauti, rangi, ladha, hali ya kibailoia ya wanyama na mimea na hali ya kijamii ya kiuchumi na hujumuisha vyote baina ya mazingira asilia na ya kimaumbile.

### **Tathmini**



Utaratibu wa ukaguzi wa mradi uliokwisha au unaoendelea. Nia huwa ni kutoa majibu ya maswali muhimu kutoka kwa watawala na kuamua thamani ya jumla, jitihada utoaji wa masomo kwa ajili ya kuboresha shughuli za baadaye mipango na maamuzi. Tathmini kwa kawaida huamua kufaa, ubora

wa matokeo, athari, uendelevu na mahusiano ya mradi na madhumuni yake. Tathmini hutoa taarifa ya kufaa ili kuwawezesha wabia na mashirika ya wafadhili kufanya maamuzi.

#### **Mwelekeo wa mfumo wa Kimantiki (LFA)**

Ni zana ya uchambuzi na usimamizi inayohusisha uchambuzi wa matatizo, wadau, kuanzisha mfumo wa kingazi kwa ajili ya kupanga madhumuni na kuteua mikakati bora ya utekelezaji. Hii inahusu zana, mazao, kusudio, lengo na uhusiano wake, pamoja na hisia za nje (hatari) ambazo zinaweza kupelekea mradi kufaulu au kushindwa. Kwa hali hii hufanikisha mipango, utekelezaji na tathmini ya mradi.

#### **Tathmini ya Athari ya Kimazingira**

Ni upimaji uliofanyika kwa kufuata utaratibu maalum kupima ikiwa au hakuna mradi ambao una madhara yoyote katika mazingira. Hii huweza kuwa na maana ya ripoti iliyoandikwa ambayo huwasilisha matokeo ya uchunguzi wa athari ya mazingira.

#### **Mchanganuo wa Kimazingira**

Huhusisha upimaji wa athari za madhara katika mazingira yaliyoathiriwa na mradi na kiwango cha mahitaji muhimu ya mradi kuwiana na sera iliyopo ya mazingira na mfumo wa sheria.

#### **Usimamizi wa Mazingira**

Ni utathmini endelevu wa athari halisi na umuhimu wa shughuli au kitu chochote katika mazingira ikiwa ni muda mfupi au muda mrefu.

#### **Uchunguzi Yakinifu**

Huu ni uchunguzi unaofanywa kuibua uthibitisho wa mwenendo sahihi wa pendekezo la mradi kulingana na mahitaji ya kiufundi, kiuchumi, kijamii, kimazingira na kifedha.

#### **Mchanganuo wa Kifedha**

Hii hujumuisha ubainishaji wa gharama za kifedha na faida ya kuendeshea mradi, kwa kawaida kwa kutumia bei ya masoko na chombo cha mchanganuo kama vile vya Faida-Fiche (IRR) na thamani ya viwango iliyopo (PV).

#### **Mwaka wa Fedha wa Madaraka Mikoani**

Hii hujumuisha mchakato wa kubainisha rasilimali sahihi na namna ya kuirodhesha kwa ajili ya kuisafirisha rasilimali hiyo hadi katika vitengo vya madaraka Mikoani katika Wilaya na ngazi za chini.

## **Athari**

Matokeo ya kitendo chochote ambacho huathiri kitu au vitu vingi vya asili, jamii au uchumi, mazingira, aidha washauri au wanufaika.

### **Athari isiyo ya Moja kwa Moja**

Ni zile athari ambazo huchochea mabadiliko katika mazingira asilia, watu, ukuaji wa uchumi, na matumizi ya ardhi.

### **Viwango vya Faida-Fiche**

Ni viwango vya faida katika uwekezaji ambapo thamani halisi iliyopo (NPV) ni sifuri

### **Hatua za Kupunguza Madhara**

Vitendo ambavyo hupunguza, kuzuia au kuondoa madhara na athari ya kimazingira ya mradi.

### **Thamani Halisi Iliyopo (NPV)**

Thamani halisi iliyopo ya uwekezaji ni thamani ya leo ya mlolongo wa malipo yajayo na mtiririko halisi wa mradi.

### **Ushiriki**

Ni mchakato ambao wadau huathiri na kutawala hisia juu ya jitihada za maendeleo na maamuzi juu ya rasilimali ambazo huwaathiri wao.

### **Mbinu Shirikishi**

Mchakato wa kupanga maendeleo ambao ni chini-juu na kinyume chake na ambao huwashirikisha wadau.

### **Kipindi cha kurudisha mkopo (PBP)**

Ni kipindi cha muda (ndani yake) ambamo fedha za uwekezaji zilizokopwa pamoja na limbikizo linalipwa bila kuathiri uendeshaji wa mradi.

### **Malengo ya Sera.**

Malengo ambayo taifa na Serikali za Mitaa inatarajia kupata kama ilivyo ndani ya miundo ya sera mbalimbali, kama vile malengo ya kuondoa umaskini kama ilivyo ndani ya mpango wa kuondoa umaskini na kuongeza uchumi Tanzania (MKUKU TA)) sera ya MPA

### **Kukabidhi Madaraka ya Kisiasa**

Ni mchakato ambapo baadhi ya watengeneza sera na wenye nguvu za kutekeleza sera wanahamishwa kutoka Makao Makuu kwenda kwenye Serikali za mitaa za Madaraka Mikoani.

### **Thamani Iliyopo (PV)**

Thamani ya sasa ya malipo au orodha ya malipo yatakayopokelewa siku zijazo, kwa kawaida hujulikana kama punguzo la thamani iliyopo ya malipo ya baadaye.

### **Kipaumbele**

Ni mchakato wa kupanga malengo ya pendekezo la mradi kidaraja katika mtiririko kwa kuanza na lengo ambalo ni muhimu zaidi kwa wanaufaika kwa kutumia tathmini sahihi ya kiufundi.

### ***Mradi***

Ni shughuli ya uwekezaji ambapo rasilimali ya kifedha hutumika kutengeneza rasilimali mtaji (mali) ambayo huzaa faida katika kipindi cha muda mrefu.

### **Ukadiriaji wa Mradi**

Hii hujumuisha tathmini ya kina ya uhusiano, na matokeo muhimu ya wazo la mradi au pendekezo kabla ya kufanya maamuzi kuidhinisha malipo ya fedha na rasilimali watu.

### **Tathmini ya Mradi**

Ni tathmini katika kipindi maalum cha mradi unaofanywa na wakala wa nje ili kupata uhusiano, ufanisi, matokeo, athari na uendelezaji kulingana na malengo yaliyoainishwa na mazao tarajiwa.

### **Kuutambua Mradi**

Ni awamu ya kwanza ya mchakato, inayoongoza kujua jinsi jambo linavyoathiri mambo kutokana na rasilimali zilizopo, uchaguzi wa malengo kutoka katika orodha ya mahitaji ya mawazo ya kimaendeleo ambayo yanaweza kuwapo na kutafsiriwa kama shughuli ya uwekezaji kibenki na kifaida.

### **Utekelezaji wa Mradi**

Ni shughuli zifanywazo tangu mwanzo hadi mwisho, kwa kulitafsiri pendekezo la mradi uliokadiriwa na kuidhinishwa kwenda katika mawazo mwonekano na utumizi kijamii na au miundo mbinu ya kiuchumi katika eneo husika.

### **Usimamiaji Mradi**

Ni shughuli ya kiutawala wa ndani itendekayo katika kipindi chote cha muda wa mradi, ikilenga kusaidia mradi kuendelea katika mkondo wake kulingana na shughuli zilizopangwa kufanyika na mazao yake.

### **Uchujaji Mradi**

Ni mchakato wa kuongoza, kutoa vipaumbele na kufanya maamuzi ya utendaji wa mradi kulingana na vigezo vilivyokubaliwa.

### **Mawanda**

Awali, utambuzi bayana wa vipaumbele muhimu vya athari ya kimazingira na kutovizingatia au kuziondoa athari zisizo muhimu au athari ambazo tayari vimeondolewa na tathmini nyingine ya athari ya kimazingira.

### **Uchujaji**

Kutambua hatua zinazohitajika za tathmini ya athari ya kimazingira katika mradi au shughuli fulani iliyopendekezwa. Ni tathmini au hukumu ya kitaalamu juu ya ukubwa wa athari yoyote katika mazingira ya utekelezaji.

Matokeo muhimu katika mazingira, humaanisha, “Kuhakikisha umuhimu, mabadiliko kinyume katika mambo ya kimaumbile ya mazingira ya binadamu yakijumuisha ardhi, maji angahewa, hali ya

hewa, sauti, harufu, ladha, hali ya kimaumbile ya wanyama na mimea na hali ya kijamii ya kiuchumi ikijumuisha mazingira asilia na ya kimaumbile.

### **Mchanganuo wa Kijamii**

Ni tathmini ya kina ya thamani ya mawazo ya mipango kuhusu kupata hali ya jamii kwa mradi ambao unaweza kuwepo, kwa kawaida ukihitaji marekebisho ya malengo ya mradi ambayo yanawiana na mahitaji ya watu wa mradi huo na pande nyingine zilizovutiwa na mradi huo.

### **Washikadau (Wadau)**

Ni wale ambao huathiriwa na matokeo ya mradi au wanaweza kuathiri matokeo ya mradi uliopendekezwa ama athari hasi au chanya.

### **Wanufaika Walengwa**

Ni watu binafsi au jumua ambao mara moja au faida ya muda mrefu wa mradi wananufaika nayo, kama vile kituo cha Afya au barabara.

### **Mchanganuo wa Kiufundi**

Upitiaji upya wa pendekezo la mradi ili kuhakikisha kwamba una madhumuni mazuri na unaonekana umeandaliwa kiufundi

**Uwazi**

Ubainishaji wa malengo katika utawala wa mchakato mzima wa mzunguko wa mradi.